

**MAELEZO MAFUPI YA MAFUNZO YA KIUFUNDI YA TEHAMA
TAREHE 18/1/2016**

- Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki (Mb)
- Mkurugenzi wa TEHAMA SERIKALINI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Ndugu Priscus Kiwango
- Mkurugenzi wa TEHAMA Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ndugu Erick Kitali
- Mkurugenzi Mtendaji, University of Dar-es-Salaam, Computing Centre Dkt. Ellinami J. Minja
- Washiriki wa mafunzo
- Ndugu Wakufunzi;
- Wageni Waalikwa;
- Wana Habari;
- Mabibi na Mabwana.
- Habari za Asubuhi!

Mheshimiwa Waziri

Nichukue fursa hii kukushukuru wewe kipekee kwa kukubali na hatimaye kujumuika nasi kwenye ufunguzi wa mafunzo haya muhimu kwa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao hapa nchini. Kwa heshima na taadhima, nichukue fursa hii kukukaribisha rasmi wewe mgeni rasmi pamoja na washiriki wote wa mafunzo haya.

Mheshiwa Mgeni Rasmi

Mafunzo haya yanalenga maafisa TEHAMA 210 waliochaguliwa kutoka Wizara zote, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafunzo haya yatafanyika kwa awamu kumi (10) kuanzia leo hadi Juni 3, 2016 katika vituo vya UCC Dar es Salaam na Dodoma. Mafunzo haya yataendeshwa na wataalamu toka UCC ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimwa Mgeni Rasmi

Mafunzo haya yamelenga maeneo yafuatayo:

1. SYSTEM DEVELOPMENT
2. CLOUD COMPUTING
3. BUSINESS CONTINUITY
4. INFORMATION SYSTEMS AUDIT
5. DATABASE MANAGEMENT
6. ENTERPRISE ARCHITECTURE
7. DEVELOPMENT, MANAGEMENT AND ADMINISTRATION OF WEBSITES AND WEB APPLICATIONS
8. NETWORK MANAGEMENT AND ADMINISTRATION
9. SERVER ADMINISTRATION AND MANAGEMENT (MICROSOFT AND LINUX)
10. MOBILE APPLICATION

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Kwa heshima na taadhima, naomba sasa nikukaribishe wewe mgeni rasmi ili aweze kutufungulia mafunzo yetu.

KARIBU SANA